# Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili

*Joviet Bulaya na Pauline Mhango*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
*jovietbulaya@yahoo.com & ngoshamhango@yahoo.com*

## Ikisiri

Ajenda ya utunzaji wa mazingira imetawala mijadala ya kitaifa na kimataifa. Baada ya kuanza kujitokeza kwa masuala ya kimazingira katika fasihi ya makundi mengine ya kijamii, fasihi ya watoto imebaki ikiwa imetengwa na kubaguliwa katika kushughulikia masuala hayo. Kwa hiyo, fasihi ya Kiswahili hususani utanzu wa fasihi ya watoto imejikuta ikipewa msisitizo usioridhisha na watunzi pamoja na wahakiki katika kuwasilisha na kuchambua masuala ya kiikolojia. Makala haya yanakusudia kushughulikia suala hilo kwa kuzingatia misingi mahususi ya Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia. Uhakiki wa Kiikolojia ni nadharia inayochambua kazi za kifasihi kwa kujikita katika vipashio vya uhusiano au muumano na pengine utegemeano baina ya binadamu na mazingira. Kwa mujibu wa nadharia hii, utamaduni wa jamii una nafasi kubwa ya kujenga mtazamo na mienendo inayoathiri matumizi ya mazingira kwa namna mbalimbali. Ili kutimiza lengo la makala haya, tumechambua data kutoka hadithi teule za watoto zilizobuniwa na kuandikwa katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania. Tumeanza kwa kutoa utangulizi, kufasili dhana ya mtoto, kuelezea misingi ya nadharia iliyotumika na kisha kuwasilisha data pamoja na uchambuzi wake.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya makundi mahususi ya kijamii hutumiwa na jamii kwa madhumuni kama ya kutoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya kiakili na kijamii kwa kundi husika. Kwa mfano, fasihi ya watoto inatumiwa na jamii kama njia mojawapo ya kuathiri na kubadili mienendo yao kwa lengo la kuwafanya wafuate mielekeo na mienendo inayotakiwa katika jamii (Pinsent, 2005). Kuna njia mbalimbali za kuwasilishia aina hii ya fasihi kwa watoto ikiwa ni pamoja na matumizi ya vitabu vya hadithi. Makala haya yanalenga kuchunguza ujitokezaji wa maudhui ya utunzaji wa mazingira katika hadithi za Kiswahili za watoto. Katika kufikia adhima hiyo, makala haya yatatumia misingi ya Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia. Aidha, sehemu hii imeangazia ufafanuzi wa dhana za msingi zilizotumika katika

makala haya, zikiwamo, dhana ya mtoto, mazingira pamoja na ikolojia. Dhana hizi zimetolewa ufafanuzi na kuonesha jinsi zilivyotumika kufikia malengo yetu.

## 1.1 Dhana ya Mtoto

Katika siku za hivi karibuni, mijadala kuhusu dhana ya mtoto imeongezeka zaidi kutokana na kukua kwa mahusiano baina ya jamii ulimwenguni kupitia mifumo mbalimbali ya kiutandawazi. Hoja hii inashadidiwa na Jones (2009) anayedai kuwa mitazamo inayokinzana kuhusu fasili ya dhana hii inachochewa kwa kiasi kikubwa na masuala kadhaa ikiwa ni pamoja na mielekeo inayokinzana kisiasa, kiutamaduni na utambulisho wa kijamii au kieneo. Vilevile, mitazamo hiyo inachochewa na nia ya kutaka kumhusisha na kumjumuisha mtoto katika masuala ya kisheria na haki za binadamu. Mathalani, asasi kama Umoja wa Mataifa katika *the United Nations Convention on the Rights of the Child* (1989), (Bisht, 2008) pamoja na Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (2016) zinafasili dhana ya mtoto kuwa ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Hata hivyo, African Child Policy Forum-ACPF, (ht.) wanafafanua kuwa kuna baadhi ya nchi ambazo umri wa mtoto uko chini zaidi kinyume na matamko na mikataba ya kimataifa iliyotajwa hapo juu. Kwa mfano, katika nchi za Libya na Malawi mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 16. Katika nchi ya Somalia, mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 15. Aidha, kuna nchi ambazo ukomo wa umri wa mtoto kabla ya kuingia utu uzima uko juu zaidi ya miaka 18. Mathalani, katika nchi za Burundi na Ivory Coast, mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 21. Kwa hiyo, dhana ya mtoto inapatiwa fasili kutegemeana na mitazamo na tamaduni za jamii husika. Mitazamo hii inawekewa misingi yake na asasi za kijamii kama vile dini, mila pamoja na desturi za wanajamii.

Koech na Njoroge (2018) wanaeleza kuwa katika siku za hivi karibuni, thamani ya mtoto katika jamii za Kiafrika imeshuka kwa kiwango kikubwa. Kushuka kwa thamani ya mtoto kijamii kunaenda sanjari na kupuuzwa pia kwa masuala yanayohusu ustawi wa mtoto katika maisha yake ya sasa na ya baadaye. Hali hii ni kikwazo cha mwendelezo, ustawi na uthabiti wa jamii nyingi za Kiafrika. Mabadiliko ya kimtazamo kumhusu mtoto yameathiri pia mtazamo wa jamii hizo kuhusu maana ya mtoto. Matukio mbalimbali ya kidunia na kijiografia yameathiri kwa kiasi kikubwa jamii asilia, miundo ya kijamii na taasisi zake. Kuhusiana na hali hii, Sanz-Caballero (2013) anaeleza kwamba kuna uwezekano

wa kujitokeza kwa mabadiliko pia juu ya mtazamo wa watu kumhusu mtoto unaosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sanz-Caballero anasisitiza pia kwamba mitazamo kuhusu haki za mtoto inayodhihirika kupitia vipengele vya kiutamaduni, inaweza kubadilika. Kwa sababu hiyo, kuna hatari ya kumpuuza na kumsahau mtoto kuwa ni sehemu muhimu ya mwendelezo wa jamii na masuala yote yanayobeba mustakabali wa jamii kama vile utamaduni, mazingira, uchumi, maendeleo pamoja na utambulisho wa kijamii kupitia vipengele vya lugha na fasihi. Fasihi kama nyenzo mojawapo ya kueneza utamaduni wa jamii huakisi mitazamo ya kijamii kuhusu masuala anuwai, likiwamo suala la dhana ya mtoto na taswira za mazingira. Hivyo, utamaduni unaojitokeza katika kazi za kifasihi na katika nyenzo nyinginezo unaukilia namna ya kuyachunguza masuala mbalimbali ya kijamii kama vile dhima ya hadithi za watoto katika uchukulizi wa mazingira asilia, uhifadhi, utamaduni na nafasi ya hadithi hizo katika kujenga utu wa watoto.

Katika jitihada za kutatua utata wa fasili ya dhana ya mtoto, Bakize (2014) na Lyimo (2014) wanabainisha kuwa dhana hii yafaa ifafanuliwe kwa kuzingatia vigezo mahususi. Vigezo hivyo ni mamlaka za kiserikali, jamii, imani, umri, sifa za kibiolojia pamoja na mitazamo ya mashirika ya kitaifa na kimataifa, hasa Shirika la Kazi Duniani. Wanaeleza kuwa kwa kuazingatia mtazamo na vigezo mahususi vilivyoainishwa na asasi hizi, mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Hivyo, vigezo vinavyoainishwa na asasi zilizotajwa vinasaidia wanajamii kote ulimwenguni kumtazama mtoto kwa namna moja. Pamoja na maelezo yaliyotolewa, makala haya yanamchukulia mtoto kuwa ni mtu yeyote mwenye umri kati ya miaka 6-15 kama inavyosisitizwa na Mgani (2013). Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, hiki ni kipindi ambacho mtoto anakuwa amejengeka kiakili kiasi cha kuelewa anachofundishwa au anachoona na kukisikia. Pia, kipindi hiki cha kirika hutumiwa na jamii nyingi kuwajenga watoto kimalezi na kimakuzi. Kwa hiyo, ni kipindi ambacho mtoto anaweza akajifunza masuala kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa ufanisi zaidi.

Mgani (2013) anaeleza kuwa kanuni ya mkwezo wa kimaadili hulenga kukuza maadili kwa kuzingatia mwelekeo chanya katika jamii na kwamba kwa kuwa watoto ni sehemu muhimu ya mhimili wa asasi za kijamii, lazima wathaminiwe. Hata hivyo, dhana ya mtoto haieleweki kwa namna moja miongoni mwa jamii ulimwengni. Kama wanavyoeleza Lyimo (2014) na Bakize (2014), dhana ya mtoto ni miongoni mwa dhana ngumu kuzipatia fasili majumui. Wakati wa kujaribu kuipatia dhana hii fasili changizi, wataalamu mbalimbali wanajaribu pia kujibana katika

vigezo vitokanavyo na muktadha wa kifasili. Hata hivyo, vigezo vinavyonuiwa na wanazuoni kuondoa utata au ugumu wa kufasili dhana ya mtoto vinazua matatizo zaidi kwa sababu vigezo hivyo vinatofautiana. Mathalani, wakati Bakize (2014) anatumia vigezo vya mamlaka za kiserikali, mashirika ya kitaifa na kimataifa hasa Shirika la Kazi Duniani, Lyimo (2014) anatumia vigezo vya kijamii, kiimani, kiumri na kibiolojia. Tofauti za vigezo vinavyotumiwa na wanazuoni kupata fasili faafu ya dhana ya mtoto vinaelekea kuifanya dhana ya mtoto kutoeleweka bayana. Hali hii inaelekea pia kuwa chanzo cha kutofahamika vizuri kwa fasihi ya watoto, jambo linaloweza kuchochea pia kutopewa uzito kwa fasihi yao, hasa fasihi inayoangazia masuala ya kijamii kama utunzaji wa mazingira. Utata wa kupata fasili moja ya dhana ya mtoto unaweza pia kutatiza uelewekaji wa umuhimu wa mahusiano ya makundi mbalimbali likiwamo kundi la watoto kiikolojia. Kimsingi, maelezo haya yanaashiria kuwa kuna pengo la kinadharia katika kueleza dhana ya mtoto, na katika kuwahusisha watoto na masuala ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Makala haya yanaona kuwa pengo hilo linaweza likakabiliwa kwa kutumia misingi maridhawa ya Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia.

Aidha, Kahigi (1995) anafafanua kuwa kwa mujibu wa Mradi wa Vitabu vya Watoto (CBP) nchini Tanzania, vitabu vya fasihi ya watoto vinapatikana katika ngazi tatu. Ngazi ya I inajumuisha watoto wanaoweza kuanza kusoma elimu ya awali mpaka darasa la pili, ngazi ya II inajumuisha wanafunzi wa darasa la tatu na la nne, na ngazi ya III inajumuisha wanafunzi wa darasa la tano, sita na la saba. Vilevile, Kahigi anabainisha kwamba uainishaji wa ngazi hizi za vitabu vya watoto unawiana na ngazi za kielimu nchini Tanzania. Mtazamo wa Kahigi (1995) na CBP unaweka kando kundi kubwa la watoto wanaoweza kuwa kidato cha kwanza mpaka cha tatu ambao bado wako kwenye kundi rika la watoto. Aidha, mtazamo huu unakanganya kwa sababu kuna watoto na hata watu wazima waliokosa fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu wanaoweza kutumia vitabu vilivyohusishwa na ngazi hizo tatu hapo juu lakini kiumri hawako katika kundi la watoto. Hivyo, ipo haja ya kulitazama jambo hili kwa mtazamo angavu zaidi. Makala haya yanaona kuwa mtazamo wa kuwahusisha watoto na masuala ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira unaweza kuwa mwafaka zaidi.

Akijielekeza katika muktadha wa utunzi na uandishi wa vitabu, Madumulla (2001) anafasili dhana ya mtoto kwa kigezo cha elimu na umri. Madumulla anaeleza kuwa mtoto ni mtu mwenye umri wa kwenda shule ya chekechea hadi kufikia umri wa kuhitimu elimu ya msingi, yaani darasa la saba hususani miaka mitatu

hadi kumi na mitano. Ufafanuzi wa Madumulla hautusaidii kuelewa dhana ya mtoto katika miktadha ya kijamii, kiumri na kielimu. Katika mazingira ya sasa, ni rahisi kukuta mtoto mwenye miaka kumi na tano anasoma elimu ya sekondari. Kwa hiyo, kigezo cha umri ni thabiti zaidi katika kufasili dhana ya mtoto kwani kinazingatia makuzi ya binadamu kiakili kuliko kutawaliwa na ngazi za kielimu ambazo mtu yeyote katika jitihada za kutafuta elimu rasmi anaweza kuzipitia bila kujali umri wake. Utafiti uliofanywa na waandishi wa makala haya unakubaliana na fasili ya Mgani (2013) kuhusu dhana ya mtoto kuwa ni mtu mwenye umri kati ya miaka 6-18 bila kujali kuwa yuko katika mfumo wa elimu rasmi au la. Katika umri huu, mtoto anaweza kusoma na kuelewa vitabu vilivyotungwa kwa kuzingatia kiwango cha makuzi ya akili yake.

## 1.2 Dhana ya Mazingira

Dhana ya mazingira imepewa fasili tofautitofauti na wataalamu kutegemeana na msisitizo wa kiweledi unaozingatiwa na mfasili. Thirmurthy (2004) anaeleza kuwa wanazuoni wengi wanakubaliana kuwa mazingira ni jumuisho la vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai vinavyomzunguka binadamu. Aidha, anaendelea kufafanua kuwa mazingira ni pamoja na maliasili zinazopatikana katika maeneo tunayoishi, hewa, ardhi na maji, uhai wa mimea na wanyama, hali ya kijamii pamoja na kiuchumi. Mambo mengine ni hali inayoshawishi maisha ya wanadamu na jumuiya zao, majengo, miundombinu, mashine na mambo mengine yaliyoundwa na wanadamu, maada ngumu, vimiminika, harufu, gesi, joto, sauti, mitetemo, mnururisho wa moja kwa moja au ule unaotokana na shughuli za kibinadamu pamoja na ama sehemu moja au mchanganyiko wa mahusiano ya vyote vilivyotajwa hapo juu.

## 1.3 Dhana ya Ikolojia

Kietimolojia, dhana ya ikolojia inatokana na mizizi miwili ya maneno ya Kigiriki oikos (nyumba) na logy (sayansi ya au taaluma ya) (Odum, 1975). Kwa hiyo, ikolojia ni taaluma inayochunguza uhusiano baina ya viumbe na mazingira yao. Kuna uhusiano thabiti kati ya binadamu, mimea, wanyama na mazingira asilia. Hali ya mazingira ya huo wakati huukilia aina na kiwango cha hadhi ya maisha ya viumbe hai. Aidha, kiwango cha ubora wa maisha ya viumbe hai kinaukilia hali ya mazingira asilia katika kipindi husika. Huu ndio uhusiano wa kiikolojia. Uhusiano wa kiikolojia hujitokeza kwa sura mbalimbali. Kwa mfano, maisha ya binadamu yanategemea mimea kwa kuwa ndiyo inayozalisha gesi ya oksijeni

ambayo ni muhimu katika mfumo wa upumuaji. Mimea ni kivutio cha mvua ambayo ni hitaji la msingi kwa ajili ya shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji. Mimea nayo inategemea kwa kiasi kikubwa mbolea inayozalishwa na wanyama kama binadamu ambao huzalisha kiwango kikubwa cha hewa ya ukaa ambayo ni malighafi muhimu kwa mimea katika mchakato wa usanisi wa chakula chao.

## 1.4 Fasihi na Mazingira

Dhima ya kazi za kifasihi katika jitihada za kutunza mazingira haijapewa uzito katika makongamano na mijadala ya kitaaluma na kiweledi (Ogechi, 2015). Pengine mtazamo juu ya kazi hizi unabakia kuzichukulia kama masimulizi yasiyo na mashiko na uwezo wa kushughulikia utunzaji wa mazingira. Kwa mtazamo wetu, hoja na ushahidi wa sayansi asilia kuhusu uharibifu na uchafuzi wa mazingira vinapewa nafasi kubwa kiuzito kuliko hoja za sayansi za jamii kama historia, anthropolojia, lugha na fasihi. Vilevile, ujumi wa kifasihi uliomo kwenye kazi za fasihi unadhihirisha jinsi tamaduni za jamii zinavyoumba, kudhibiti na kuukilia mitazamo, imani, elimu na ufahamu kuhusu mazingira.

Pamoja na ujumbe uliomo katika kazi za fasihi kuhusu usawiri wa masuala ya mazingira, uzito unaoelekezwa katika utunzi, ufundishaji na uhakiki wa kazi za fasihi hususani fasihi ya watoto hauwiani na uzito wa ujumbe huo kiutunzaji wa mazingira. Sababu zinazochangia hali hiyo zinatokana na ulegelege wa mfumo na utekelezaji hafifu wa sheria zinazohusu haki za watoto, tamaduni na imani potofu zinazoelekezwa katika baadhi ya makundi ya kijamii kama vile watoto, walemavu na wanawake. Kwa upande mwingine, tunaweza kusema kuwa hali hii inasababishwa na kutoelewa nafasi ya fasihi ya makundi haya ya kijamii katika harakati za kupambana na kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira na ama kuleta ukombozi kwao wenyewe. Tunapolichunguza jambo hili na kulihusisha na muktadha wa fasihi ya Kiswahili, tunabaini kuwa vitabu au fasihi ya Kiswahili kwa watoto na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla havipewi nafasi kama msingi wa kuwajenga watoto kisaikolojia, kiroho na kijamii ili waweze kuwa raia bora wanaozingatia utunzaji wa mazingira katika siku za baadaye. Ari na moyo wa kupenda na kuyathamini mazingira kwa watoto vinaweza kujengwa na kukuzwa kupitia kazi za fasihi zinazohusu mazingira. Matatizo yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi yanayochochewa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira yangeweza kudhibitiwa kwa kutumia mafunzo na elimu inayopatikana katika fasihi ya watoto, simulizi na andishi.

Fasihi ni njia mwafaka inayoweza kudhibiti mienendo, tabia na matendo yasiyofaa katika jamii. Jamii inayokusudia kuwa na kizazi bora kinachothamini misingi ya utu, usawa, upendo na usalama wa mazingira yake, inapaswa kutilia mkazo matumizi ya fasihi ya watoto katika kufundishia mambo muhimu ya kijamii, likiwamo suala la mazingira. Watoto wanapopewa fursa ya kutangamana na fasihi za namna mbalimbili (simulizi na andishi) hujifunza misingi muhimu ya kimazingira, kijamii, kiutamaduni, kisiasa na kisheria. Heise (2016) anatoa maoni kwamba fasihi ina uwezo wa kujenga utamaduni utakiwao kuhusu utunzaji wa mazingira wenye manufaa kwa binadamu na viumbe wengine. Aidha, tatizo la mabadiliko ya tabianchi litokanalo na uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni matokeo ya hali halisi ya jamii na uelewa wake kuhusu utunzaji wa mazingira.

Kutokana na maoni hayo, ni makosa kuendelea kuamini kuwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira vinaweza kutatuliwa kwa mbinu za sayansi asilia peke yake. Tabia ya kutojali thamani ya mazingira miongoni mwa wanajamii inachipukia zaidi katika mienendo inayopaliliwa na tamaduni zisizojali nafasi ya fasihi katika kuendeleza ustawi wa mazingira. Tatizo la uchafuzi na uharibifu wa mazingira linaweza kudhibitiwa kwa kutumia taaluma za sayansi za jamii kama fasihi ya watoto inayotokana na utamaduni wa jamii husika. Fasihi hii inaweza kutumika kuwafundisha watoto na kuwajenga kiutu na kuona umuhimu wa kutunza mazingira yao. Kwa njia hii, watoto na wanajamii watajiepusha na tamaduni hatarishi katika ustawi na usalama wa mazingira. Tahadhari na mabunio ya kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi huukiliwa na namna jamii ilivyo au inavyopaswa kuwa. Kwa hiyo, utamaduni wa jamii unaweza kuchochea au kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kwa kuzingatia kuwa fasihi ya watoto inawasilisha masuala ya kiutamaduni, tunaweza kuitumia kuakisi na kutathmini upya hatua za kuchukua ili kujenga mustakabali endelevu wa mazingira. Aidha, kwa mujibu wa Ogechi (2015) na Bakize (2017) suala la kuihisha fasihi na mazingira, na suala la kuzingatia ufaafu wa fasihi ya watoto katika mazingira yamekuwa na mwelekeo hasi katika jamii kutokana na mambo mawili: (i) kutofautiana kwa jamii mbalimbali kuhusu dhana ya mtoto; na (ii) kutotumika vyema kwa nadharia mwafaka ya kuchambulia masuala ya kimazingira katika fasihi, yaani Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia. Ili kuziba pengo hili, makala haya yamechunguza ujitokezji wa maudhui ya utunzaji wa mazingira kwa kuzingatia hadithi za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Katika kutekeleza jukumu hili, tumetumia misingi mahususi ya Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia. Misingi hiyo imefafanuliwa vyema katika sehemu ifuatayo.

## 2.0 Misingi ya Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia

Uchambuzi wa matini teule za kifasihi zilizotumika katika makala haya umeongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia. Nadharia hii ilianzia huko Marekani na mwasisi wake ni Glotfelty (1995). Kuanzishwa kwa nadharia hii kulichochewa na nia ya kuchambua bunilizi kuhusu mazingira zilizotungwa magharibi mwa Marekani. Uhakiki wa kiikolojia uliibuka kufuatia mabadiliko ya tabianchi yaliyosababishwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Kuhusu misingi ya nadharia hii, Mulokozi (2017) anabainisha kuwa uhakiki wa kiikolojia ni mkondo wa uchambuzi wa kazi za fasihi unaochunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na mazingira. Kwa hiyo, uhakiki wa kazi za kifasihi kwa mtazamo wa kiikolojia unayachukulia mazingira kama ajenda ya msingi katika uhakiki wake (Glotfelty, 1995: xviii). Vilevile, uhakiki wa kazi za kifasihi kiikolojia unamakinikia dunia kama mada kuu na kuchambua sifa kuihusu dunia na uhusiano wake na viumbe na maumbile yaliyomo katika dunia kupitia matini za kifasihi. Aidha, kwa kuzingatia uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa mtazamo wa nadharia hii, maudhui yanayohusu uhusiano baina ya binadamu na mazingira asilia ndiyo yanayotawala katika kazi za fasihi. Halikadhalika, Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia inasisitiza kwamba utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Glotfelty, 1995). Hii ina maana kuwa uhakiki wa kiikolojia unachunguza jinsi binadamu, utamaduni na mazingira vinavyoathiriana. Kwa kuwa utamaduni unahusu namna watu waishivyo katika maisha yao ya kila siku, uhakiki wa namna hii ni njia mwafaka ya kudhihirisha mienendo ya matumizi na uhusiano baina yao na mazingira waishimo. Utamaduni ni njia inayowatofautisha watu kijamii na ni njia ya kujibainisha kutoka katika makundi yao ya kijamii. Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia inachambua pia dhima ya mazingira katika kuukilia utamaduni wa jamii katika kipindi mahususi cha kihistoria pamoja na mila na desturi zinazohusishwa au zisizohusishwa na hali ya mazingira na sababu za kufanya uamuzi huo.

Mara nyingi, matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu. Kwa mujibu wa Glotfelty (1995), hali hii inatokea pale shughuli za kibinadamu zinapoharibu uwezo wa kawaida wa dunia kuwezesha uendelevu wa mifumo ya kiikolojia. Uhakiki wa kazi za fasihi kiikolojia ulikusudia kutatua changamoto za uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Nchini Tanzania kuna matatizo ya kimazingira kama vile ukame, mafuriko, kuongezeka kwa gesijoto na kutoweka kwa baadhi ya

bioanuwai na viumbelishe katika uso wa dunia. Matumizi ya nadharia hii katika makala haya yamezingatia uwezo wake wa kutoa elimu, kujenga uelewa na ufahamu muhimu juu ya utunzaji wa mazingira. Ili kuchambua kazi za kifasihi, vipengele mbalimbali vya kisanaa kama vile wahusika, mandhari na dhamira vimejadiliwa na kuhusishwa na suala la mazingira.

## 3.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Makala haya yalikusudia kujadili usawiri wa maudhui ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika kazi za kifasihi, hususani hadithi za watoto. Hadithi zilizochambuliwa zinapatikana katika vitabu vifuatavyo: *Kavuta Mrina Asali* (Sekibaha, 2006), *Mbawala na Nchi ya Ujinga* (Mrikaria na Omari, 2006), *Mtoto Mrembo* (Mrikaria na Omari, 2006) pamoja na *Watoto Wanaofanana* (Mrikaria na Omari, 2006). Uteuzi wa vitabu hivi ulizingatia upatikanaji wa maudhui, wahusika wa kimazingira na mandhari kuhusu masuala ya kimazingira pamoja na mwaka wa utunzi. Vitabu hivi vimetungwa katika kipindi ambacho mijadala kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira imepamba moto katika jamii ya Kitanzania na jamii nyingine ulimwenguni.

Aidha, kwa kuongozwa na misingi ya nadharia iliyofafanuliwa kwenye kipengele kilichotangulia, tunaona kuwa taasubi za kimazingira zimefumbatwa na imani za jamii kuhusu mazingira. Kadhalika, tumebaini kuwa wasanii wanapoyasawiri masuala haya hutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na dhamira, mandhari pamoja na wahusika.

Kupitia uchambuzi huo, waandishi wamefanikiwa kubainisha namna hadithi za Kiswahili za watoto zinavyowasilisha maudhui ya utunzaji wa mazingira. Katika uchambuzi wetu, tumebainisha kategoria tatu za masuala ya kimazingira, yaani uharibifu wa kutokukusudia, uharibifu wa kukusudia na uharibifu wa mazingira unaopewa msukumo na shughuli zinazofanywa na wahusika katika harakati zao za maisha ya kila siku.

### 3.1 Wahusika

Uchunguzi wetu umebaini kuwa hadithi za watoto zimesheheni wahusika wa kimazingira wanaohusishwa na mazingira pamoja na binadamu. Huu ni uhusiano wa kiikolojia ambao unathibitisha msisitizo wa Nadharia ya Uhakiki wa Kiikolojia kuwa binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana; ustawi wa kimoja kutegemea kwa

kiasi kikubwa kuwapo kwa kingine. Mathalani, katika kitabu cha *Kavuta Mrina Asali* panasawiriwa uhusiano wa kiikolojia baina ya binadamu na mazingira yake. Katika hadithi zote nne zinazopatikana katika kitabu hiki, masuala ya kiikolojia yamewasilishwa kwa namna mbalimbali. Uthibitisho wa hali hii unajitokeza katika hadithi ya "Kisa cha Paka Kuishi kwa Binadamu." Kutokana na hadithi hiyo, inadhihirika kwamba matumizi mazuri ya mazingira yanamnufaisha binadamu na viumbe wengine. Mathalani, kutokana na mazingira, Mzee Kavuta aliweza kupata asali iliyoipatia familia yake lishe bora na fedha. Vilevile, Mzee Kavuta aliuza ziada ya asali na nta na kumwezesha kulipa mahari kwa ajili ya watoto wake walipofikia umri wa kuoa.

Aidha, katika hadithi ya "Kisa cha Paka Kuishi na Binadamu", mhusika fisi anatumika kisitiari kuwakilisha watu wanaoharibu mazingira wanapotafuta mahitaji yao. Tamaa ya fisi inasababisha uharibifu wa mazingira kwa kuchoma na kueneza moto unaoathiri wanyama wengine. Kutokana na moto uliowashwa na fisi, paka anaungua na kulazimika kubadili makazi yake ya asilia hivyo kwenda kuishi kwa binadamu. Kisa hiki kinasawiri hali halisi inayoyakabili mazingira, binadamu na viumbe hai wengine. Ni jambo la kawaida kusoma au kusikia katika ripoti mbalimbali kuwa viumbe wa aina fulani wamehama makazi asilia kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa au uharibifu wa makazi yao ya awali, chanzo kikubwa kikiwa ni binadamu. Uchomaji moto kama uliofanywa na fisi, unasawiri kwa kiasi kikubwa tabia za baadhi ya watu na jamii kupenda kuchoma moto katika mazingira ili kurahisisha uwindaji au shughuli za kilimo. Huu ni uharibifu wa mazingira unaochochewa na msukumo wa kujipatia mahitaji yao. Katika hadithi ya "Kisa cha Paka Kuishi na Binadamu" na ile ya "Mzee Kavuta Atumbukia Kisimani" msanii anasema yafuatayo:

> Siku moja fisi alipita karibu na moto uliokuwa umebanikwa nyama. Fisi alitamani sana nyama ile. Mate yakamdondoka mithili ya mtu aliyekamuliwa limao au ndimu mdomoni. Bahati mbaya mtu aliyebanika nyama hakusogea hata hatua moja, aliendelea kuigeuzageuza kwa umahiri mkubwa. Fisi aliendelea kusubirisubiri na kuhangaika kwa kificho aweze kupata kinofu. Hatimaye nyama ilikuwa imeiva kabisa tayari kwa kuliwa. Ndipo yule mtu alipoondoka

> kidogo kwenda kutafuta majani na kamba ya kufungia ile nyama. Fisi akanyata! Akaona amepata kumbe amepatikana. Alirukia kipande alichodhani kilikuwa ni mfupa uliozungukwa na mnofu kumbe kilikuwa kipande cha ukuni chenye moto mkali. Kama ilivyo kawaida yake akakimbia nao kuelekea porini ili kufaidi uhondo ule. Masikini! Ule moto ulimuunguza fisi barabara. Alipokuwa akikimbia kwa maumivu kuelekea porini alidondosha makaa ya moto. Paka bila kujua aliyakanyaga akaungua vibaya katika wayo wake wa kulia. Alipata maumivu makali sana. Akachechemea kuelekea kwenye nyumba iliyokuwa pale msituni akakutana na mzee aliyekuwa anaitwa Kavuta. Mzee Kavuta alimhurumia sana yule paka … Hakutamani tena kuishi porini na akina fisi, wabadhirifu na wasiotosheka (uk. 2-3). Biashara ya asali na nta ilimtajirisha sana Mzee Kavuta. Mzee huyu alihifadhi fedha yake kwenye mtungi. Familia yake walikuwa na siha njema kutokana na ubora wa lishe ya asali. […]. Mzee Kavuta alipata fedha nyingi sana hasa kwa vile asali ilitumika pia kulipa mahari vijana walipopata wachumba pale kijijini na vijiji vya jirani (uk. 12).

Katika dondoo hili, mwandishi wa hadithi anadhihirisha uhusiano wa mazingira asilia na viumbe wengine pamoja na binadamu. Hadithi hizi zinawasilisha dhamira ya manufaa ya mazingira kwa ustawi na uendelevu wa maisha ya vizazi vijavyo. Kupitia hadithi hizi, unatolewa ujumbe kwamba jamii inapaswa kuzingatia matumizi salama ya mazingira ili kujihakikishia fursa ya kunufaika nayo siku zote.

Vilevile, katika hadithi hizi tunajifunza kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira badala ya kuyaharibu kutokana na uroho na matendo hatarishi. Kutokutunza mazingira kunawaathiri watu kwa ukame na ukosefu wa mahitaji muhimu kama chakula na maji. Ukosefu huu wa chakula na maji unasawiriwa kwa kuadimika kwa asali katika tarafa aliyoishi Mzee Kavuta. Hali hiyo ilisababishwa na ukosefu wa maji na maua ambavyo ni malighafi zinazotumiwa na nyuki katika utengenezaji

wa asali. Kuhusiana na hali hii, msanii anaeleza, "Kutokana na ukame ule, asali ilipatikana kwa nadra sana kutokana na nyuki kukosa maua ya kujitengenezea asali na nta" (uk. 4). Kwa hiyo, kutokana na dondoo hilo hapo juu, uharibifu wa mazingira unaathiri kwa kiwango kikubwa msawazo wa kiikolojia kiasi cha kuhatarisha maisha ya viumbe hai na mustakabali wa mazingira.

Kuonekana kwa viumbe na miondoko au mielekeo yao wanapojitokeza katika mazingira, kunaashiria hali ya mazingira ilivyo. Wahusika kama ndege na vipepeo wanasawiri hali ya kudhoofu kwa mazingira kiasi cha kutokidhi mahitaji ya viumbe hawa kama inavyojitokeza katika 'Hadithi ya Kisa cha Binadamu Kuishi na Paka'. Uchoraji wa wahusika ndege na vipepeo katika hadithi hii unawasilisha dhamira ya umuhimu wa kutunza uoto wa asili. Uoto huo una manufaa mengi kwa binadamu, ikiwamo kupatikana kwa matunda na uzalishaji wa hewa ya oksijeni ambayo ni muhimu kwa afya na uhai. Vilevile, ni chanzo muhimu cha mvua na mhimili wa vyanzo vya maji. Maji, mimea na madini anuwai ni vyakula na virutubisho vya afya za viumbe na mazingira kwa ujumla. Kwa hiyo, uharibifu wa aina yoyote wa uoto wa asili unahatarisha maisha ya viumbe hai na mazingira na kunayumbisha msawazo wa mfumo wa kiikolojia. Mathalani, miti ikikauka haiwezi kutoa maua ambayo ni malighafi muhimu kwa nyuki kutengeneza asali. Kwa binadamu, asali ni lishe na ni tiba ya magonjwa mbalimbali na kwa nyuki asali ni akiba ya chakula chake wakati wa kiangazi. Uharibifu wa mazingira wa aina yoyote unachochea kutoweka kwa baadhi ya viumbe kutokana na kukosa mahitaji yao ya msingi. Kutoweka huko kunasababisha athari mbalimbali kama zinavyoelezwa katika matini hii:

> Miti ilikauka na kupukutisha majani. Ikawa kama imekauka kabisa. Sehemu zilizokuwa na vijito vilivyotiririka maji kutokea milimani zilikuwa ndizo pekee zilizokuwa na majani na maua. Hata ndege na vipepeo walionekana wakirukaruka pamoja kuashira kuwepo kwa uhai na matumaini katika eneo lile. Kutokana na ukame ule, asali ilipatikana kwa nadra sana kutokana na nyuki kukosa maua ya kujitengenezea asali na nta (uk. 4).

Kinachosisitizwa katika dondoo hili ni kwamba uhai na ustawi wa viumbe unategemea kwa kiasi kikubwa uhai na usalama wa mazingira hai na mazingira ufu. Mathalani, milima ni chanzo muhimu cha maji na ni kivutio cha upatikanaji wa mvua. Kwa hiyo, kiikolojia viumbe hai wanahusiana na mazingira wanamoishi. Dondoo lifuatalo linasawiri vema uhusiano huo:

> Alianza kujiuliza ni jinsi gani angeweza kuingia mle ndani ya tundu la mti hata asielewe la kufanya. Baadaye alipata wazo zuri kuwa ashuke atafute majani ya mti uitwao mlenda na mshubiri ili ajipake mwili mzima ili ateleze moja kwa moja na kuingia tunduni (uk. 6).

Katika nukuu hapo juu tunaona jinsi mazingira asilia yanavyochangia kupatikana kwa asali aliyokuwa akihitaji Mzee Kavuta. Kutokana na matini iliyodondolewa, Mzee Kavuta aliposhindwa kuingia katika pango ili arine asali, aliamua kupaka mwili wake mlenda uteleze hatua iliyomwezesha kuingia katika lile pango lenye asali nyingi kwa wepesi. Mhusika huyu ametumika kudhihirisha umuhimu wa mazingira katika ustawi wa maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Hadithi ya "Wivu Unaua" inaonesha kuwa wivu na migogoro ya kijamii inachangia kuharibu mazingira na maisha ya binadamu na viumbe wengine. Uharibifu wa mazingira unakuwa silaha ya maangamizi ya binadamu mwenyewe baada ya kutekeleza uharibifu huo. Wahusika wanaojikuta katika mazingira ya kushindania mahitaji yanayofanana au yanayoelekeana na wakati huo rasilimali wanayoishindania ikiwa haikidhi mahitaji yao au haigawanyiki kwa namna yoyote ile, kwa vyovyote vile huingia katika migogoro. Katika hadithi ya "Wivu Unaua", mahusiano ya ukewenza yametumika kuwasilisha hali hii. Katika hadithi hii msanii anaeleza kuwa:

> Hapo zamani za kale palikuwa na mzee mmoja aliyeoa wake wawili, Bi mkubwa na Bi mdogo. Mke wa kwanza alikuwa na watoto wawili na mke wa pili alikuwa na mtoto mmoja. Yule Bi mkubwa alikuwa hampendi yule mtoto wa mke mwenziwe. Basi siku moja alimchukua yule mtoto wa mke mwenziwe

> mpaka msituni. [...]. Walipofika msituni yule mama akachimba shimo na kusema, "Kila mtoto apande juu ya mti halafu aruke ndani ya shimo hili. Yule mtoto wa mke mwenziwe ndiye aliyeamrishwa aruke kwanza. Basi aliporuka tu akaangukia shimoni. Wale watoto wake hawakuruka. Hivyo akawaamrisha washuke na wakarudi nyumbani (uk. 19).

Katika dondoo hili, shimo ni sitiari ya shughuli za kibinadamu zisizozingatia utunzaji, uhifadhi na utumiaji wa mazingira kiuendelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Aidha, watoto ni taswira ya fursa na haki ya kutumia mazingira bila kuzua migogoro baina ya watu na ni taswira ya vizazi vijavyo. Hapa maudhui ya utunzaji wa mazingira yamewasilishwa kwa njia ya sitiari na taswira.

Jamii isiyotunza mazingira inaishi maisha ya kibinafsi pasipo kujali kuwa watoto watakaozaliwa siku zijazo watahitaji kuendesha maisha yao kupitia mazingira hayo. Migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima au migogoro baina ya wawekezaji na wananchi wa kawaida imesawiriwa vema katika hadithi ya "Wivu Unaua". Kutokana na usawiri huo, tunabaini kuwa, uchafuzi wa mazingira unasababisha kuyumba kwa mfumo wa kiikolojia na kuhatarisha maisha ya viumbe hai wakiwamo watoto. Kama inavyodhihirika katika dondoo hapo juu, watoto ni wahanga wakuu wa uharibifu wa mazingira wa makusudi unaojitokeza katika jamii. Aidha, uharibifu huo unahatarisha utengemavu wa mazingira yenyewe.

### 3.2 Mandhari

Mandhari ni dhana inayotumika kurejelea mazingira au mahali pnapohusishwa na kazi ya fasihi au tukio maalumu katika kazi ya fasihi. Utamaduni wa matumizi ya mazingira kijamii unaweza kudhihirika pia kupitia uteuzi wa madhari ya kazi ya fasihi. Vitendo vinavyohatarisha maisha ya binadamu vinaweza kujengewa misingi yake kutegemeana na utamaduni wa matumizi ya mazingira asilia (Glotfelty, 1996). Katika hadithi ya "Mwanamke Mwenye Wivu", inadhihirishwa tabia ya kusudio la mauaji kwa sababu ya kuoneana wivu. Kichocheo kikubwa cha tabia hii ni uroho na tamaa ya kumiliki rasilimali zote. Uharibifu wa makusudi wa mazingira unatumiwa kuhatarisha maisha ya watoto ambao ni wahanga wakuu

wa uharibifu wa mazingira kutokana na uwezo wao mdogo wa kukabiliana nao. Katika ukurasa wa 6 tunaelezwa yafuatayo:

> Zamani sana palikuwako mtu aliyeoa wake wawili. Mke wa kwanza alizaa binti wa madaha, lakini yule wa pili alizaa mtoto asiye na sura nzuri. Siku moja alimchukua Bi mkubwa kwa safari ya juma moja. Walipoondoka, huku nyuma Bi mdogo alichimba shimo kubwa pale mlangoni pao, alilifunika kwa manyasi. Ikafika wakati yule Bi mdogo akamtuma yule mtoto mzuri wa Bi mkubwa kwenda ndani kuchota maji. Yule msichana alipopita mlangoni alianguka na kutumbukia mle shimoni. Yule Bi mdogo akakimbia haraka na kulifukia lile shimo.

Katika dondoo hili, Bi mdogo amechorwa kusawiri ubinafsi na wivu wa binadamu katika matumizi ya mazingira. Kitendo cha kuchimba shimo mlangoni kinatafsiriwa na makala haya kama taswira ya matumizi mabaya ya mazingira kwa kiasi cha kuhatarisha ustawi wa vizazi vijavyo. Bi mdogo anafanya vitendo vya kikatili kwa kutumia mazingira kumuangamiza mtoto pasipo kujua kuwa kwa kufanya hivyo anajiangamiza yeye mwenyewe. Maisha ya binadamu na vizazi vyake yanategemea mazingira. Ufanisi wa mtu mmoja unategemea mchango wa watu wengine. Haya ni mahusiano ya kiikolojia baina ya watu wenyewe kwa wenyewe na jinsi wanavyotegemeana na mazingira yao. Hadithi ya "Mwanamke Mwenye Wivu" ambayo inapatikana katika *Mbawala na Nchi ya Ujinga* imedhihirisha madhara ya kutotunza na kutumia mazingira kiuendelevu. Uhusiano wa kiuhasama na tabia ya kuoneana wivu kupitia matumizi ya mazingira vinamwangamiza mwanadamu. Kilio cha mtoto aliyefukiwa katika shimo kinamvuruga mtoto wa Bi mdogo kimaono kila anaposikia kilio cha mtoto wa Bi mkubwa. Hii ni kwa sababu mtoto aliyefukiwa shimoni haelekezi lawama kwa Bi mdogo bali analalamika akimlenga mtoto wa Bi mdogo. Kilio cha mtoto wa Bi mkubwa ni mwangwi wa kilio cha mazingira yanayoharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu katika jitihada za kutafuta maendeleo. Kwa hiyo, katika hadithi hii, mtoto ametumika kama taswira ya kimazingira kusawiri uharibifu wa makusudi wa mazingira na namna viumbe wanavyoteseka na uharibifu huo.

Vilevile, kilio hiki kinawakilisha mwangwi wa madhila ya kizazi kijacho na dunia na hali yake ya baadaye kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayokua kwa kasi ya kutisha. Aidha, ni ishara ya rai ya watoto kutaka kujumuishwa katika kukabiliana na changamoto za kijamii na kimazingira. Hivyo, hadithi za Kiswahili kwa watoto zinasawiri masuala ya kiikolojia kuhusu mazingira kama yanavyojitokeza katika mazingira yetu katika kipindi hiki cha janga la mabadiliko ya tabianchi.

Kwa upande wa kitabu cha *Mtoto Mrembo*, hadithi ya "Mtoto Mrembo", mtoto mrembo anachorwa kitaswira kama mazingira na rasilimali. Kutokana na hadithi hii, tunabaini kuwa mazingira yana nafasi ya msingi katika kuamua mienendo na tabia za wahusika katika kazi za fasihi. Katika hadithi hii, mazingira yaliyotunzwa yanasawiri tabia njema miongoni mwa watoto wetu siku za usoni lakini mazingira yaliyoharibiwa yanaukilia tabia na mienendo isiyofaa kijamii na kwa mazingira yenyewe. Tabia za ufisadi, uongo, usaliti, ubaguzi na upotoshaji zinajitokeza katika hadithi hii kama taswira na mwangwi wa tabia zisizofaa kujenga uhusiano mwema kiikolojia miongoni mwa watu, mazingira na viumbe vingine. Mathalani, mkasa wa Limando unamwacha Limando bila mama baada ya kudanganywa kumtumbukiza mama yake kisimami kwa ahadi ya kupewa chungu. Kwa bahati mbaya, hata alipotekeleza hila na unyama alioagizwa na mama yake mdogo, hakutengenezewa chungu kama alivyoahidiwa. Dondoo lifuatalo linadhihirisha hali hii:

> Alipofika nyumbani akamwambia mama yake mdogo kuwa amekwisha kumtumbukiza mama yake kisimani. Mama yake mdogo alijibu, "Rudi hukohuko! Ni nani aliyekutuma ukamtumbukize mama yako kisimani? (uk. 11).

Katika hadithi ya "Mtoto wa Mfalme na Mtoto wa Masikini", Mtoto wa Mfalme anaokolewa kifoni na Mtoto wa Maskini. Katika ukurasa wa 15 wa kitabu cha *Mtoto Mrembo*, msanii anaeleza:

> Alitokea Mtoto wa Mfalme na Mtoto wa Maskini. Watoto hao walikuwa marafiki sana. Siku moja walipatana kwenda kuwinda. Kufika huko yule Mtoto wa Maskini akapatwa na usingizi, alakala chini ya

> mti. Akiwa usingizini akasikia sauti ikimwambia, "Ee bwana! Mtoto wa Maskini! Mtakaporudi nyumbani mwenzio, Mtoto wa Mfalme ataliwa na punda wa mfalme hadi afe." Walipokuwa wakirudi nyumbani, kabla hawajatembea sana punda akaja kutaka kumla mtoto wa mfalme. Mtoto wa Maskini akampiga risasi punda huyu na kumuua.

Wanapotumika kisitiari, watoto wanaotajwa katika dondoo hapo juu wanatumika pia kuwasilisha fundisho kuwa tunapaswa kuyapenda, kuyalinda na kuyapigania mazingira yetu kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Kiikolojia, urafiki wetu binadamu ni mpana ukijumuisha sisi binadamu wenyewe kwa wenyewe, mazingira hai na mazingira ufu. Kwa kuzingatia umuhimu wa mazingira, tunapaswa pia kujitoa kwa moyo kupigania ustawi wake kwa kuwa uhai na ustawi wetu pamoja na viumbe wengine unategemea mazingira asilia. Kwa hiyo, mahusiano baina yetu, mazingira na viumbe wengine yanadhibitiwa na uthabiti wa mfumo wa kiikolojia.

Tamaduni za jamii zina athari chanya au hasi kuhusu uhai wa mazingira. Jamii zinazofanya ibada zake katika maumbile asilia kama milima, mito, majabali, mapango, maziwa, mabwawa na miti mikubwa huchangia utunzaji na uhai wa mazingira hayo. Kutoweka kwa tamaduni kama hizi kunahatarisha uhai wa mazingira. Katika kitabu cha *Mtoto Mrembo*, kisa cha "Mtoto wa Mfalme na Mtoto wa Masikini" kinasawiri mifano ya mielekeo ya kiutamaduni katika matumizi ya mazingira. Katika kisa hiki, mazingira yanaonesha uwezo wa kutatua matatizo yanayomkabili binadamu na kumpatia mahitaji ya kila siku.

Mazingira asilia katika kisa cha "Mfalme na Mtoto wa Maskini" yanampatia kitoweo kila anapokwenda kuwinda. Aidha, mazingira haya yanaokoa uhai wa Mtoto wa Mfalme kwa kufunua hatari iliyomkabili kwa njia ya mti unaoongea. Kila ilipotokea hatari yoyote dhidi ya Mtoto wa Mfalme, mti huu ulimtahadharisha Mtoto wa Maskini. Huu ni udhihirisho wa falsafa ya Kiafrika inayobainisha imani na ibada za Waafrika kufanyika katika maumbile ya kidunia kama miti mikubwa. Dondoo lifuatalo linathibitisha hali hii:

> Alitokea Mtoto wa Mfalme na Mtoto wa Maskini. Watoto hao walikuwa marafiki sana. Siku moja walipatana kwenda kuwinda. Kufika huko yule

> Mtoto wa Maskini akapatwa na usingizi, akalala chini ya mti. Akiwa usingizini akasikia sauti inayotoka katika mazingira ikimwambia, "Ee Bwana! Mtoto wa Maskini! Mtakaporudi nyumbani mwenzio, Mtoto wa Mfalme ataliwa na punda wa mfalme hadi afe". [...]. Siku ya pili wakaenda tena kuwinda. Kwa bahati walifanikiwa kupiga ndege. Wakakaa chini ya mti wakapumzika. Yule Mtoto wa Mfalme akalala. Mtoto wa masikini alipolala akasikia sauti ya kimzimu katika mazingira ikimwambia, "Mtoto wa Maskini! Mimi nakuonea huruma sana; maana jogoo wa baba ya rafiki yako atakuja na kumuua palepale. [...]. (uk. 15).

Sauti inayopazwa na mandhari ni wito wa kisitiari unaosisitiza umuhimu wa mazingira katika maisha ya viumbe hai na msawazo wa kiikolojia kwa ujumla. Kwa hiyo, imani zinazokitwa katika mazingira zinaweza kuchangia katika utunzaji wa mazingira. Hii ni kwa sababu, ibada za wanajamii na majibu ya maombi ya shida zao yanatolewa na maumbile ya kimazingira. Hivyo, jamii haiwezi kuharibu mazingira na maumbile ya kimazingira kwa kuwa ni msingi wa utatuzi wa shida zao za kimwili na kiroho.

Jamii kupitia makundi yake maalumu kijinsia, kiumri, kiweledi, kimamlaka na uwezo wa kiuchumi inadhibitiwa na mahusiano ya kiikolojia kama mfumo. Vilevile, tamaduni nazo zinadhihirisha uhusiano wa kiikolojia baina yake na mazingira kwa namna kwamba tamaduni rafiki kwa mazingira zitachochea uthabiti na ustawi wa mazingira. Tamaduni zisizofaa huchangia kuharibu mfumo wa kiikolojia wa mazingira asilia. Kwa upande mwingine, hali yoyote katika mazingira inaweza kuathiri utamaduni wa jamii na kuamua aina ya matumizi ya mazingira hayo. Makala haya yamechambua hadithi za fasihi ya Kiswahili ya watoto sita (6). Makala yamewasilisha na kuchambua vipengele viwili vya kifani vikihusishwa na namna vinavyosawiri maudhui ya utunzaji wa mazingira.

## 4.0 Hitimisho

Kwa kuwa athari za uchafuzi na uharibifu wa mazingira zinagusa makundi yote ya kijamii, mapambano dhidi yake yanapaswa kuwa jumuishi. Katika nchi ya Tanzania, kuna makundi ya kijamii ambayo hayapewi kipaumbele katika vita hivi. Watoto, watu wenye ulemavu na wanawake wana nafasi na mchango mkubwa katika kukuza ufahamu juu ya masuala ya kimazingira. Tatizo lililopo ni kwamba tamaduni zetu zinayabagua makundi haya kwa imani kuwa mchango wake ni mdogo. Mapambano dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni ya kiikolojia. Kila mmoja ana nafasi na umuhimu wa pekee katika mapambano haya. Kutokana na hadithi zilizochambuliwa ni dhahiri kuwa mapambano haya yanatakiwa kuwa shirikishi bila kujali jinsia, umri, elimu, hali ya ulemavu, mamlaka au uwezo wa kiuchumi alionao mtu.

## Marejeleo

Bakize, L. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Bisht, R. (2008). "Who is A Child?: The Adults' Perspective within Adult-Child Relationship in India". *Interpersona* 2(2), 151-172. Jawaharlal Nehru University, India.

Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (Tanganyika Law Society) (2016). *Mtoto na Haki Zake. Sheria katika Lugha Rahisi.* Dar es Salaam: Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara (Tanganyika Law Society).

Glotfelty, C. (1995). "Introduction. *The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*." Katika Cheryll Glotfelty and Harold Fromm (wah.). The University of Georgia Press: Athens.

Heise, U.K. (2016). (Mh.) *Literatures, Cultures and the Environment*. Palgrave: Macmillan.

Jones, M. (2009). "The Development of Culture Identity in Early Childhood Settings." Leicester: De Montfort University.

Koech, P.K. na Njoroge, P.N. (2018). "Changes in the Traditional African Concept of the Child and Childhood: The Aftermath with Reference to Kenya." Mt. Kenya University.

Lyimo, E.B. (2014). "Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau nchini Tanzania." Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mgani, T. (2013). "Usawiri wa Mhusika Mtoto katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Ngome ya Mianzi* na *Marimba ya Majaliwa*." Tasnifu ya M.A. Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mulokozi, M.M. (2017). Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu. Dar es Salaam: KAUTTU.

Odum, E.P. (1975). *Ecology*. New Delhi, Bombay na Calcuta: Oxford na IBH Publishing Co. PVT Ltd.

Ogechi, I.U. (2015). "Nature in Nigerian Children's Literature: An Appraisal of Selected Verses". Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Ahmadu Bello, Zaria.

Pinsent, P. (2005). "Language Genres and Issues: The Socially Commited Novels." Katika. Kimberly Reynolds (mh). Modern Children's Literature. New York: PalgraveMacmillan. Kur. 191-197.

Sanz-Caballero, S. (2013). "Children's Rights in a Changing Climate: A Perspective from the United Nations Convention on the Rights of the Child." *Ethics in Science and Environmental Politics* Vol. 13: 1–14, 2013.

United Nations. (1989). *The United Nations Convention on the Rights of the Child.* New York: United Nations.

The African Policy Forum. (ht). Definition of the Child: The International/ Regional Legal Framework. www.africanchildforum.org/clr/... otherdocumentsharmonasation.1.en.pdf. Imesomwa tarehe 17/02/2020.

Thirmurthy, A.M. (2004). *Principles of Environmental Science, Engineering and Management*. Mumbai: Shroff Publishers.

**Orodha ya Vitabu vya Hadithi Teule**

Mrikaria, S. E. na Omari, S. (wah.) (2006). *Mtoto Mrembo*. Dar es Saalam: TUKI.

Mrikaria, S. E. na Omari, S. (wah.) (2006). *Watoto Wanaofanana*. Dar es Saalam: TUKI.

Mrikaria, S. E. na Omari, S. (2006). (wah.) *Mbawala na Nchi ya Ujinga*. Dar es Saalam: TUKI.

Sekibaha, L. A. (2006). *Kavuta Mrina Asali*. Dar es Salaam: TUKI.